Toleo Maluum - Mei-Juni 2007

UKWELI WA MAMBO

Toleo Maalum la Kauli ya Nguvu ya Hoja, Ndugu Mwandawiro Mghanga

Propaganda za kunipaka matope ya uhalifu hazitafua dafu

Tangu tarehe 24 Mei nimekuwa nikipigwa propaganda chafu na vyombo vya habari, polisi na wale wanaodhibiti nguvu za dola leo. Habari zimeenezwa kote nchini ati ninatafutwa na polisi ili kuandika taarifa kuhusu kundi haramu la Mungiki. Lengo la propaganda hizo ni kunichafua, kunifanya nionekane mtu mbaya mbele ya watu wa Wundanyi, nchini na duniani kwa ujumla. Je, kweli mimi ni mhalifu, ni mtu anaehusika na uzoroteshaji wa usalama nchini? Nasema la, mimi si mhalifu wala sihusiki na Mungiki. Mimi ni kiongozi ninaejiheshimu na ninaeheshimiwa nchini na kimataifa. Watu wa Wundanyi mna sababu ya kuendelea kusimama nami. Msitishwe na mtu au kitu. Nitawaeleza ukweli ulivyo maana penye ukweli uongo hujitenga.

Kwanza kiini cha uongo na dhuluma dhidi yangu sasa. Ikumbukwe kwamba imebaki miezi sita tu ndipo kuwe na uchaguzi mwingine wa kitaifa. Uchaguzi huu utaamua kuhusu nani atakuwa diwani, mbunge au rais wa Kenya. Si ajabu kwamba kampeni tayari zimechacha kote nchini na pia katika Eneo Bunge letu la Wundanyi. Ni harakati, ni mapambano. Kwa ujumla, kitaifa ni mapambano kati ya wanaongoza serikali sasa na upinzani ambao unajipanga kuchukua madaraka kutoka kwa serikali iliyoko kupitia kwa kura zitakazopigwa Disemba.

Mimi niko kwa upande wa mageuzi yenye lengo la kuleta uongozi mpya nchini. Uongozi utakaoondoa vikwazo vyovyote vinavyotuzuia kufanya maendeleo kwa haraka na kuboresha maisha ya watu wengi wa Kenya. Ninataka kura zipigwe serikali iliyoko iondoke madarakani kwani imefeli mtihani. Pamoja na kasoro zingine ambazo nitazieleza wakati ukiwadia, serikali iliyoko imekataa kutupa katiba mpya kama ilivyokuwa imeahidi. Ukabila katika kugawanya vyeo na rasilimali umezidi huku ufisadi ukitia fora. Wakati tunaambiwa ati uchumi umeimarika, bei za bidhaa muhimu kama sukari, mafuta taa, unga, n.k., zimepanda mno. Mashirika ya umma yanabinafsishwa na kuuziwa matajiri wa kienyeji na nje bila kutilia manani masilahi ya kitaifa na ya wengi.

Mapambano yaliyoko ni kati ya siasa za kimaendeleo na zile zenye lengo la kuturudisha tulikotoka. Kati ya ukweli na uongo, mwangaza na giza. Ingawa mimi ninatambua na kutetea haki za wapinzani za kuhubiri kuhusu siasa za amani, wapinzani wangu wanakitaka kiti cha ubunge kwa vyovyote vile

Ukosefu wa kazi unaongezeka huku pengo kati ya matajiri na maskini likizidi kupanuka. Watu wachache nchini ni matajiri kupindukia huku wengi wakiwa mafukara wanaokufa kwa njaa, maradhi, ukosefu wa nyumba na shida na dhiki za kila aina. Usalama kote nchini umezoroteka mno, watu wanachinjwa na kuawa na majambazi usiku na mchana hasa katika mikoa ya Kati, Magharibi, Nairobi na Bonde la Ufa. Wakati haya yote yakifanyika inakuwa ni propaganda chafu za kulaumu viongozi wa upinzani kama mimi badala ya kukamata na kuchukulia hatua majambazi wanaowaua watu, kuharibu mali zao na kusababisha hofu na wasiwasi nchini.

Kwa sababu hii ifikapo Disemba nimesema itakuwa vema serikali iliyoko ikiondolewa madarakani na kupisha serikali nyingine itakayoleta suluhu ya matatizo haya yote

yanayoikumba nchi yetu sasa. Maana tulipoondoa utawala wa Kanu na Moi angalau tulipiga hatua mbele kimaendeleo na kidemokrasi. Sasa tumeanza kukwama tena. Ndiyo maana kwa vile sasa serikali iliyoko imekua kikwazo cha kwenda mbele basi ni muhimu tujitayarishe kupiga kura za kuiondoa ili angalawa tupate mwanya wa kupiga hatua mbele zaidi. Ni muhimu nchi izidi kupiga hatua mbele kidemokrasi, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na huku haki za kila mwananchi na jimbo zikikua.

Huku Wundanyi, mapambano ni kati yangu na wale wanaotaka kiti cha ubunge cha Wundanyi, wapinzani wangu. Nae Mkuu wa Wilaya ya Taita - Taveta amejiingiza katika kampeni za wapinzani, kwa sababu zinazojulikana. Mapambano yaliyoko ni kati ya siasa za kimaendeleo na zile zenye lengo la kuturudisha tulikotoka. Kati ya ukweli na uongo, mwangaza na giza. Ingawa mimi ninatambua na kutetea haki za wapinzani za kuhubiri kuhusu siasa za amani, wapinzani wangu wanakitaka kiti cha ubunge kwa vyovyote vile.

Propaganda chafu zinazotangazwa na magazeti, redio na televisheni ati ninatafutwa na polisi kuandika taarifa ati kuhusu tuhuma za kuhusika na kundi haramu la Mungiki zinakusudiwa kuharibu jina langu na kunipaka matope mbele ya watu wa Wundanyi ninaowawakilisha na washirika wangu wa kisiasa kitaifa na kimataifa.

Wako tayari kusema chochote kile juu yangu alimradi waniharibie jina tu. Ikiwa watanihusisha na siasa za Mkoa wa Kati za Mungiki, kwao wanaona ni sawa tu. Wanashangilia huku jina langu likiharibiwa na polisi, magazeti, redio na televisheni ati mimi ndie ninaejua kuhusu mambo ya Mungiki. Kana kwamba mimi ni Waziri wa Usalama! Kana kwamba hiyo shida ya Mungiki ipo Wundanyi tangu niwe mbunge! Kana kwamba matatizo ya usalama wa nchi hii yanasababishwa na Mwandawiro wa Mghanga!

Kwa ufupi, wapinzani wangu wana chuki, wivu na uhasama juu yangu. Kwa nini? Kwa sababu ninaiheshimu kazi mliyonipa ya ubunge na ninaifanya ipasavyo. Tena kwa uaminifu sana. Sijashiriki ufisadi ama wizi wa mali ya umma. Pia, najulikana kwa kupigania mageuzi ya kimaendeleo na nimekuwa sauti inayotambulikana kitaifa na kimataifa ya kupigania demokrasi, haki
na maendeleo ya kiuchumi, kijamii na
kitamaduni. Haya yote natenda kwa uhodari nikiongozwa na ukweli tu.

Wundanyi na Taita – Taveta kwa ujumla, niko katika msitari mbele wa kupigania haki za Wadawida za kufaidi kutokana na rasilimali zao za ardhi, mbuga za wanyamapori, maji, misitu na madini. Nimekuwa na wananchi kupinga dhuluma, ufisadi, na hali ya kutokuwa na uwazi na uwajibikaji katika uongozi wa serikali Taita – Taveta, Wundanyi.

Ndiyo kwa maana nimekuwa nikipigania Katiba Mpya ya Bomas ambayo itasambaza mamlaka ya uongozi na usimamizi wa rasilimali kutoka Nairobi hadi wilayani, na kutupa mfumo wa majimbo tunaolilia Pwani siku zote. Kwa sababu hii pia nilikuwa katika msitari wa mbele wa harakati za Chungwa za kupinga katiba mbovu ya Ndizi - na shukrani wananchi daima kwa kuitika mwito sahihi wa kuelekea kwa katiba mpya, katiba ya msingi wa Bomas.

Nimedhihirisha msimamo huu kwa maswali ninayouliza bungeni na mchango wangu katika hoja na miswada bungeni. Aidha, msimamo wangu ulionekana bayana nilipoongoza maandamano ya wananchi wa Taita – Taveta kuhusu mambo haya. Nikiwa mbunge, nimeweka masilahi ya wananchi wa Wundanyi na Taita – Taveta mbele. Ndiyo maana nimekataa kushawishiwa ili niwasaliti wananchi walionichagua. Fauka ya haya, tangu niwe mbunge Wundanyi tumefanya maendeleo ambayo hayajawahi kuonekana hapo awali. Tumefaulu kufanya haya pamoja na hujuma zote zinazofanywa na afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Taita – Taveta.

Kutokana na haya yote ninafahamu kuwa nimefanya uadui na wale wote Wundanyi na nchini wanaopinga haki, ukweli na maendeleo ya wengi. Na kwa vile wana mamlaka wataweza kutumia pesa, vyombo vya dola na propaganda dhidi yangu. Na proganda ni silaha ya adui tangu kale na zamani.

Propaganda chafu zinazotangazwa na magazeti, redio na televisheni ati ninatafutwa na

polisi kuandika taarifa ati kuhusu tuhuma za kuhusika na kundi haramu la Mungiki zinakusudiwa kuharibu jina langu na kunipaka matope mbele ya watu wa Wundanyi ninaowawakilisha na washirika wangu wa kisiasa kitaifa na kimataifa. Zina lengo la kujaribu kunifanya nionekane ninahusiana na mambo ya ujambazi na ugaidi. Maadui wangu wanalenga kuwafanya watu wa Wundanyi wakose imani nami kisha ndipo vibaraka wao wachaguliwe.

Lakini mimi najua kuwa wananchi wa Wundanyi watasimama nami kwani sina makosa na wala sijawakosea. Ninasulubiwa kutokana na ushujaa wa kutetea haki na ukweli wala siyo kwa uhalifu. Nami siogopi, niko tayari kwa chochote kile hata kifo. Bora nisimame na haki na ukweli kutetea utu wangu na wa kila mtu nchini na ulimwenguni.

Hebu niwafahamishe kwamba nilisikia habari ati ninatafutwa na polisi juu ya Mungiki niliposoma gazeti la *Standard* asubuhi ya Alhamisi 24 Mei nikiwa Kisii ambapo niliandamana na ndugu Raila Odinga anaepigania uraisi wa nchi yetu. Tangu Jumatano hadi Jumamosi jioni nimekuwa nikisafiri ndani ya gari mashuhuri la Raila aina ya Hammer huko Kisii, Sotik, Buret, Bomet na Kericho. Nilikuwa nikihutubia mikutano ya hadhara nikimpigia debe Raila. Na kila siku inatangazwa kwamba Mwandawiro anatafutwa na polisi – na siku zote hizo sikuwa mafichoni, nilikuwa kadamnasi ya polisi, waandishi wa habari na raia! Isitoshe, hata nilikuwa nikionekana kwa televisheni na kupigwa picha nikiwa na ndugu Raila na viongozi wengine. Inawezekanaje polisi washindwe kunitia mbaroni wakati huu wote ikiwa walikuwa na haja nami?

Tena, niliposoma tu ati ninatakikana na polisi, nilipiga simu nyumbani kwangu Nairobi na Werugha na pia afisini Nairobi na Wundanyi kujua kama kweli ninatakikana na polisi. Ndipo nikajulishwa kuwa hawakuwa wamepata mawasiliano yoyote kutoka kwa polisi. Nikangoja siku nzima polisi wanipigie simu, wala hawakupiga. Je, ningelijipeleka polisi mwenyewe bila kuitwa kwa kuwa tu imeandikwa magazetini na kutangazwa redioni na televishenini? Hata ng'ombe haijipeleki kichinjioni.

Ndiyo kwa sababu niliporudi jijini Nairobi kutoka Kericho mnamo Jumapili tarehe 26 Mei nilishauriana na mawakili wangu kuhusu mambo haya. Nilikuwa na lengo la kwenda nyumbani kwangu moja kwa moja. Lakini mawakili wakanishauri nisifanye hivyo maana polisi watanikamata na kunifungia kizuizini ambapo nitateswa kwa jina la kuhojiwa. Wakanikumbusha kwamba seli za polisi bado hazijabadilika, ni zilezile za hali mbaya ya kutesa kila anaekamatwa na polisi.

Mawakili wakanishauri nisubiri kwanza waende kortini kuitisha korti iagize polisi waeleze ninatakiwa kituo gani cha polisi, lini na wakati gani ili niende polisi nikiandamana na mawakili wangu. Hivyo ndivyo mbunge wa Juja, Kabogo, alivyofanya na ndiyo kwa maana hakukamatwa na kufungiwa kama wanasiasa wawili George Nyanja na Adolf Muchiri. Basi wakati huu nikiandika niko nyumbani kwangu, bado nasubiri mawakili na maagizo ya mahakama.

Hata viongozi wa sasa wa serikali, mkiwemo mawaziri, wamewahi kuhusiana kwa njia moja ama nyingine na baadhi ya wanachama wa Mungiki, ingawa si lazima katika hali ya uhalifu. Kwa hivyo, kujifanya kuwa Mungiki imezuka ghafla bin vu na ati Mwandawiro na wengine wachache tu ndiyo wana habari kuhusu Mungiki ni unafiki mkubwa kuliko wa mafarisayo

---

Lakini je, ninajua nini kuhusu Mungiki? Kwanza, hebu nieleze kwamba ni muhimu ikumbukwe kuwa Mungiki imekuwa maarufu Kenya kwa muda mrefu. Wanachama wa Mungiki pia wamekuwa wakiandikwa magazetini, kusikika kwa redio na televisheni, kuonekana kwa mikutano ya kisiasa Nairobi, Mkoa wa Kati na wa Bonde la Ufa na kadamnasi ya vyama visivyo vya kiserikali tangu enzi za Rais Msitaafu Daniel Arap Moi. Mijadala kuhusu Mungiki inaendelea kila mara.

Hata viongozi wa sasa wa serikali, mkiwemo mawaziri, wamewahi kuhusiana kwa njia moja ama nyingine na baadhi ya wanachama wa Mungiki, ingawa si lazima katika hali ya uhalifu. Kwa hivyo, kujifanya kuwa Mungiki imezuka ghafla bin vu na ati Mwandawiro na wengine wachache tu ndiyo wana habari kuhusu Mungiki ni unafiki mkubwa kuliko wa mafarisayo.

Pili, nimemjua Maina Njenga, anaesemekana kuwa kiongozi wa Mungiki tangu mwaka wa 1998 nilipokuwa Katibu Mkuu wa chama cha Safina. Nilimfahamu na wengine katika harakati za kisiasa na mikutano ya vyama visiyo vya kiserikali Nairobi. Sikumjua kama mhalifu na wala sijahusiana nae vingine, maana mimi si mhalifu na sijampata akifanya uhalifu.

Tatu, mwaka uliyopita Maina Njenga na jamaa yake walikuja afisini kwangu bungeni kunifahamisha kuwa mali yao, ikiwa ni pamoja na nyumba na ardhi iliyoko Kitengela imevamiwa na kukaliwa na polisi kinyume cha sheria. Wakaniomba niwasadie kudai haki yao. Nikiwa mbunge, ninatunga sheria za kitaifa na vilevile nina wajibu wa kitaifa pamoja na kwa eneo bunge langu la Wundanyi. Hivyo, basi watu wengi wa sehemu mbalimbali na wa kuwakilisha masilahi tofautitofauti nchini hunijia wakiniomba niwasilishe malalamiko au matatizo yao bungeni. Huwa wakieleza kuwa mimi ni mbunge wao pia, kwani wananifahamu kama shujaa wa haki za wadhulumiwa nchini.

Tusije tukawacha wahalifu wajisalimishe kwa kusingizia Mungiki kila mara. Tutahadhari na kuvunja haki za binadamu Nairobi, Mkoa wa Kati na kote nchini kwa jina la kupambana dhidi ya uhalifu. Kwani nakariri, mtu yoyote yule awe Mungiki awe nani hana haki ya kuvunja sheria na kufanya vitendo vya kigaidi na kiharamia. Na huu ni ukweli wa mambo.

Na shujaa si mwoga. Haikuwa ajabu basi kwa Maina na jamaa yake kuja kwangu. Na mara mbili bungeni nikazungumza kuhusu Maina na haki yake iliyokuwa imevamiwa na polisi kinyume cha sheria. Maswali yote yalijibiwa na aliekuwa waziri msaidizi katika afisi ya Rais, marehemu Mirugi Kariuki, ambae pia aliwahi kuwa wakili wa Maina Njenga.

Nne, nimemtembelea Maina Njenga gerezani na kortini mara kadhaa. Hilo nimefanya wazi mbele ya maafisa wa magereza na polisi. Kwani mimi si Judasi wa kukana mtu wakati amepatwa na mashaka.

Basi huu ndiyo ukweli wa mambo. Ukweli ambao nimeueleza polisi. Bali haya yote hayanifanyi kuwa mwanachama wa Mungiki au mhalifu. Kwani daima inalaani vikali vitendo vyovyote vya uhalifu. Hasa nasikitika na kuomboleza na wale wote, polisi na raia, waliopoteza maisha yao kutokana na genge za wahalifu. Mtu yoyote yule awe Mungiki awe polisi, awe waziri awe nani hana haki ya kuvunja sheria. Aidha, katika kukabiliana na uhalifu, ni muhimu watuhumiwa wakamatwe, washtakiwe na kuhukumiwa kwa matendo halisi ya uhalifu wao kulingana na sheria na siyo kwa dhana tupu. Kwani dhana ikiingilia kati haki hupotea na wahalifu wa kweli hushangilia. Halafu wananchi wasiyo na hatia wanaumia. Kama kiongozi na raia mwema nina haki na jukumu la kutoa shauri hili kwa serikali na vyombo vya usalama.

Tusije tukawacha wahalifu wajisalimishe kwa kusingizia Mungiki kila mara. Tutahadhari na kuvunja haki za binadamu Nairobi, Mkoa wa Kati na kote nchini kwa jina la kupambana dhidi ya uhalifu. Kwani nakariri, mtu yoyote yule awe Mungiki awe nani hana haki ya kuvunja sheria na kufanya vitendo vya kigaidi na kiharamia. Na huu ni ukweli wa mambo.

Mwisho, propaganda dhidi yangu, zikiwa ni pamoja na kuniondolea ulinzi, hazitaninyamazisha wala kusuluhisha tatizo la kuzorota kwa usalama nchini. Kwani mimi ni raia kama raia yoyote yule Kenya. Sote tunahitaji amani na usalama. Ni lazima serikali iliyoko isuluhishe tatizo la kuzorota kwa usalama nchini bila maonevu au tetesi. Na huu ni ukweli wa mambo. **SERE YA MLUNGU IKANYE NENYO KARI KOSE!!**!